

Sheria za Kiislamu katika Zama Hizi

Katika sehemu nyingine ya mjadala wangu, kuna masuala mengine mengi ya kujadiliwa lakini hapa nitayataja kwa muhtasari tu. Uislamu una mfumo mahsusi wa utungaji wa sheria. Ajabu ya mfumo huo ni kuwa sheria zake zinaweza kwenda sambamba na maendeleo ya zama, na hata zinaweza kuwa ni mwongozo kwa maendeleo na wakati huohuo zikaweza kupambana na upotovu na ufisadi.

Msingi wa hoja yangu ni aya moja ya Qur'ani inayosema kwamba dini ya Kiislamu si dini iliyo mbali na maumbile na sheria (kanuni) za maumbile. Kwa sababu Mtungaji wa sheria hizo Ndiye Huyu Huyu Muumba wa maumbile. Na sheria Zake amezitunga kuambatana, kukubaliana na kwenda sambamba na alivyoviumba.

Aya yenyewe inasema:

"Basi uelekeze uso wako kwenye dini iliyo sawasawa, ndilo umbile (mahsusi) Allah alilowaumbia watu." (Qur'an 30:30)

Mwenyezi Mungu anasema kwamba dini ikiwa kama ni umbile moja inaafikiana na maumbile mengine ya Mwenyezi Mungu.

Aya nyingine inasema:

"Na vile vinavyowanufaisha watu vinakaa katika ardhi." (Qur'an 13:17)

Kwa kuwa dini ni umbile la aina ya pekee alilowaumbia kwa faida na manufaa ya watu, hivyo, ni lazima (dini) ibaki na iendeleo duniani. Hii ni kanuni ya kimsingi. Kuna vitu gani katika dini ya Kiislamu ambavyo vinaafikiana na kukubaliana na maumbile na kanuni ya kimaumbile ambavyo kuwepo kwavyo ni miongoni mwa misingi ya maendeleo na ukamilifu katika maumbile?

Miongoni mwa siri za misingi hiyo ni kuthaminiwa akili katika Uislamu. Wewe hutoweza kuona dini yoyote au kitabu kitakatifu chochote ambacho kimeipa umuhimu na thamani akili kama dini ya Kiislamu. Kwa bahati mbaya, sisi hatuwezi kuwa watangazaji wazuri kwa ajili ya dini yetu. Hakuna mzaha! Lakini wewe ukivirejea vitabu vya kifiqihi (sheria za Kiislamu) na ukitaka kutumia ijthadi (mbinu ya kutoa fatwa) ili utatue masiala ya kidini, misingi ipi utaitumia?

Bila ya shaka utaitumia misingi minne – Kitabu (Qur'ani), Sunna, Ijmaa (mwafaka wa wanazuoni) na Akili. Akili ni msingi mmoja kati ya Kitabu, Sunna na Ijmaa. Ijmaa pia ina nafasi yake mahsusi. Hii haina

maana kwamba Akili na Ijmaa viko mbali na Kitabu na Sunna. Hii ni fahari kubwa sana kuona kwamba tangu mwanzoni mwa Uislamu wanavyuoni wa Kiislamu wamesema kwamba kuna itifaki na makubaliano baina ya akili na sheria. Wameweka kanuni isemayo:

"Kila linalohukumiwa na akili linahukumiwa na sheria pia, na kila linalohukumiwa na sheria linahukumiwa na akili pia." Makusudio yao ni kuwa ikiwa akili imehukumu kitu ambacho hatuna ushahidi wake ulioandikwa, basi uamuzi huo wa kiakili unatosha kutufahamisha kwamba kitu hicho kinakubaliana na Uislamu. Kwa hivyo, hata kama hatuna ushahidi ulioandikwa, akili inatosha kuhukumu, kwa sababu kile kinachohukumiwa na sheria kinahukumiwa na akili vivyo hivyo. Hii ina maana kwamba sheria za Kiislamu hazikutungwa kwa mujibu wa mambo yasiyoeleweka au yasiyo na maana bali zimetungwa kufuatana na hekima, busara na akili; na vilevile zimewekwa kwa ajili ya maslahi na faida kwa maisha ya binadamu. Sheria za Kiislamu zinaafikiana na akili.

Uislamu ni dini ya kimantiki. Tuchukulie kwa mfano katika falsafa kuna suala moja ambalo hukumu yake haikuwa wazi kwa akili, lakini si jambo lililofichika au lisilo na maana au lisilokubaliana na akili, kama yale maneno ya Wakristo wanaosema kwamba akili na imani ni mbalimbali. Uislamu unasema kwamba akili na imani ni vitu vimoja na lazima viende sambamba na viafikiane. Hivi ni mizani katika fiqihi ya Kiislamu.

Katika mafundisho ya misingi ya Kiislamu, akili ni kitu muhimu sana. Katika Uislamu akili ni kipimo cha msingi katika kuamini, lakini kinyume chake katika Ukristo kutumia akili katika kuamini ni marufuku. Jambo hili limewafanya wanavyuoni wa Kiislamu wapate uwanja wa kutumia akili katika masiala ya kidini. Na hii ndiyo sababu ya kufanikiwa fiqihi ya Kiislamu tangu zamani. Mmewahi kusikia kwamba wakati fiqihi ya Kiislamu inapojadiliwa katika mikutano mingi ya kimataifa, inasifiwa sana kutokana na wepesi na ukunjufu wa sheria zake.

Jambo jingine ambalo ni sababu ya kusifiwa dini ya Kiislamu (kama nilivyokwisha eleza) ni kule kutojali hali na sura ya dhahiri ya maisha na badala yake kuitilia maanani roho ya maisha. Hii ndiyo sababu iliyoifanya dini ya Kiislamu ijiepushe kugongana na maendeleo ya kimaisha, kwa sababu yale maendeleo ya kimaisha yanayotegemea sayansi na teknolojia ambavyo vimeyapa maisha, sura, umbo na muundo, yananitaka mimi nitoe pesa kununua kitu ambacho kwa kweli hakina faida wala manufaa yoyote. Uislamu unasema kwamba muamala huu ni haramu. Biashara hiyo inakutaka wewe ununue mali ambayo haitakuletea faida yoyote, na kama unadhani kuna faida, basi faida hiyo haitambuliwi katika Uislamu.

Mafaqihi (wataalam wa sheria za Kiislamu) wamesema kwamba vitu ambavyo asili yake ni najisi vimeharamishwa kutumiwa katika Uislamu. Kwa hivyo, hakuruhusiwi kuuza au kununua vitu ambavyo ni najisi asilia, k.m. damu. Katika zama zile watu walikuwa wakinywa damu, hivyo, Uislamu uliharamisha. Sasa ikiwa zama zimegeuka na damu inatumiwa kwa faida nyingine kinyume na matumizi yale ya zamani wakati ilipoharamishwa, hapo Uislamu unaruhusu matumizi haya mapya ya damu ya mtu mmoja kumtia mtu mwingine, kwa mfano, mtu aliyejeruhiwa na akapoteza damu nyingi. Uislamu umesema kunywa damu ni haramu lakini haukukataza mtu mmoja kumpa damu mtu mwingine. Zamani matumizi

ya damu yalikuwa ni kula mali kwa batili lakini muamala wa sasa si batili. Kwa hivyo, ile sheria thabiti haitobadilika abadan. Sheria inasema:

"Wala msiliane mali zenu kwa batili...." (Qur'an 2: 188)

Hakuna mtu yeyote anayeweza kukataa sheria hii. Ikiwa kitu kimoja siku moja kilikuwa kikitumiwa kwa njia ambayo ilikuwa sawa na kula mali kwa batili, na siku nyingine kikatumiwa kwa njia iliyodhibitiwa ghairi ya hiyo, hapo patatokea badiliko la maudhui au hali. Maudhui ikibadilika hukumu yake hubadilika pia. Lakini hii haina maana ya kufutwa kwa sheria asilia na thabiti, kwani katika Uislamu sheria haifutiki bali maudhui tu ndiyo inayobadilika.

Katika zama zetu alikuwepo aalimu (mwanachuoni) mashuhuri sana ambaye alikuwa mtu mcha-Mungu sana, zahidi (walii) na faqihi, akiitwa Agha Sheikh Ali Zahidi Qummi. Haikosi mmewahi kusikia habari zake. Alikuwa na taasubu sana hivi kwamba alijiharamishia vitu vyote vya kigeni. Hakuwa akitumia kitu chochote cha kigeni. Kama kitambaa cha kienyeji kilikuwa kikipatikana alikuwa hanunui kitambaa cha kigeni. Alikuwa akisema kwamba maadamu vitu vinavyotengenezwa na Waislamu vinapatikana hakuna haja ya kutumia vitu vya kigeni. Alikuwa hanywi chai ya kigeni ila akinywa chai ya nchini tu. Hata sukari ya kigeni alikuwa hatumii na alikuwa akitumia zabibu badala ya sukari.

Walikuwepo Wazungu wawili, mama na binti yake ambao wote wawili walisilimu. Baadaye wawili hao wakakaa mjini Karbala (Iraq) na jirani yao alikuwa shekhe huyo. Watu kadhaa walishuhudia kwamba binti Mzungu alikuwa Mwislamu msalihina sana na alishika dini mpaka mwisho wa umri wake. Baada ya kufariki kwa mke wa Agha Sheikh Ali Zahidi, msichana huyo wa Kizungu mwenyewe akataka aolewe na Agha Sheikh Ali Zahidi. Agha Sheikh Ali akamwoa na akaishi maisha mazuri sana na mke huyo wa Kizungu. Inasemekana kwamba alipofariki mwanamke huyo hali ya Sheikh Ali iliharibika. Mtu mmoja alimwendea Sheikh 'Ali na akamwambia: "Shekhe, wewe ulikuwa ukituambia kuwa hutumii vitu vya kigeni, basi ilikuwaje ukamwoa mwanamke wa kigeni?" Sheikh Ali akajibu: "Mwanangu! Maudhui imebadilika. Mgeni huyo amekuwa Mwislamu."

Kwa hivyo, suala la kubadilika na kugeuza maudhui au hali ni suala jingine. Hebu nikutoleeni mfano mwingine.

Katika vitabu vya kifiqihi kuna mlango mmoja unaoitwa 'Mashindano na Kutunga Shabaha'. Ni sunna (mustahabu) kwa kila Mwislamu, kujifunza mashindani ya mbio za farasi ili kuweza kuwalea farasi wa mbio (resi). Inaruhusiwa kutumia pesa katika kuwafunza farasi wa mbio lakini hairuhusiwi katika kazi nyingine.

Kutunga shabaha kwa mshale ni sunna pia. Huenda mtu akahoji kwamba katika zama hizi hakuna haja kubwa ya kuwepo mada ya mashindano ya farasi na 'kutunga shabaha' kwa mshale, hivyo ifutwe kabisa. Lakini mtu akiangalia ataona kwamba mada hiyo imeandikwa kwa mujibu wa kanuni thabiti. Na kanuni yenyewe ni aya hii ya Qur'ani:

"Na waandalieni nguvu mwezavyo, na kwa farasi waliofungwa [tayari kwa vita], ili mwatishe maadui wa Allah na maadui wenu na wengineo ghairi ya wao msiowajua nyinyi, (lakini) Allah anawajua." (Qur'an 8:60)

Uislamu ni dini ya kijamii inayoutaka umma wa Kiislamu ujiandae na ujizatiti barabara kwa ajili ya kujihami. Nguvu za Waislamu zinatakiwa ziwe za kiwango cha juu kabisa. Sababu ya kuwekwa mashindano ya farasi na 'kutunga shabaha' kwa mshale ni kuwafanya wapiganaji wa Kiislamu wawe mashujaa na simba katika medani za mapambano. Maneno haya yanawapa moyo wapiganaji. Mashindano ya farasi na 'kutunga shabaha' ni kielelezo cha hiyo sheria thabiti na ya daima dawamu. Sheria hiyo haiwezi kufutwa.

Kwa maana nyingine farasi na mshale ni sura moja ya utekelezaji wa aya: ***"Na waandalieni nguvu mwezavyo, na kwa farasi waliofungwa [tayari kwa vita]."*** Wakati mashindano ya farasi na utungaji wa shabaha kwa mshale unapokuwa sunna katika jamii, hutumiwa kazi zake, lakini wakati vitu vingine huvumbuliwa badala yake, msingi wa "kuwaandalia" hubaki vivyo hivyo katika utekelezaji. Hii haina maana kusema kwamba katika utekelezaji wa amri hiyo kinachoandaliwa kiwe kitu cha aina moja daima. Kwa hivyo, kama nilivyokwishaeleza, Uislamu umeweka sheria thabiti na zisizobadilika kukidhi haja zilizo thabiti, lakini wakati huohuo umezingatia sheria nyinginezo kwa ajili ya haja zinazobadilika ambazo huambatana na sheria zilizo thabiti.

Inatosha kwa mwanachuoni wa Kiislamu mwenye kufahamu kusema kwamba katika kutekeleza sheria hii haina maana kwamba ni lazima ufanye mashindano ya farasi na 'kutunga shabaha' kwa mshale. Sasa maudhui imebadilika, hivyo sheria hii inaweza kutekelezwa vizuri kwa kufanya mashindano ya silaha na zana za kivita, k.v. bunduki, ndege za kivita za *phantom*, *MiG*, n.k. badala ya farasi na mshale.

Ni wazi kabisa kuwa kitu kinachopendelea Uislamu si mishale na pinde bali ni nguvu na ushujaa. Farasi na mishale vimetajwa kama mfano wa msingi huo wa kujizatiti.

Katika mfumo wa utungaji wa sheria za Kiislamu kuna vipengee kadhaa vinavyozipa uhai na nishati sheria za Kiislamu. Mojawapo kati ya wajibu wetu mkubwa sana ni kuivumbua hiyo nishati ya sheria za Kiislamu.

a.s.: kifupisho cha alayhis/alayhas/alayhimus salaam, m.y. amani iwe juu yake/yao.

s.a.w.: kifupisho cha sallallaahu alayhi wa-'Ali, m.y. baraka za Mwenyezi Mungu ziwe kwake na kwa ali (wazaa) wake.

Source URL:

<https://www.al-islam.org/sheria-za-kiislamu-katika-dunia-ya-kisasa-murtadha-mutahhari/sheria-za-kiiislamu-katika-zama-hizi>